


# HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Simu/Fax Na. 025-2820068  
Nukushi:025-2820068  
Barua Pepe:info@nsimbodc..go.tz.  
Tovuti: www.nsimbodc.go.tz  
Unapojibu tafadhali taja



S.L.P 688,  
MPANDA.

Kumb.Na.KTV/NDC/NDC/P.30/2/80

15.03.2018

Wananchi wote,  
**TANZANIA .**

## YAH: TANGAZO LA AJIRA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo anawatangazia wananchi wenye sifa kuomba kazi katika kada ya **Mtendaji wa Kijiji III**. Hii ni kutokana na Mkurugenzi kupokea kibali cha ajira Mbadala chenye Kumb. Na CFC 26/205/01 "F"/91 cha tarehe 22/08/2017 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala na Bora Ajira hizi zitakuwa za masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni (**permanent and pensionable**) na pia nafasi hizi ni kwajili ya halmashauri ya wilaya ya Nsimbo

### 1. MTENDAJI WA KIJIKI III (NAFASI 3)

#### Sifa za Mwombaji

- i. Awe na cheti cha kuhitimu na kufaulu elimu ya kidato cha nne / sita
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii, na Sayansi ya Jamii kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali
- iii. Awe raia mwadilifu mtanzania na mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45

#### Majukumu/KAZI

1. Afisa masuuli na Mtendaji mkuu wa Serikali ya Kijiji
2. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji
3. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya kijiji
4. Katibu wa mikutano na kamati zote za halmashauri ya kijiji
5. Kutafasri na kusimamia sera, sheria na taratibu katika ngazi ya kijiji
6. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
7. Kiongozi mkuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji
8. Kukusanya mapato ya halmashauri
9. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
10. Kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya wananchi
11. Kuwa mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo kijijini mwake
12. Pamoja na kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

## Ngazi ya Mshahara

TGS B

### Masharti kwa waombaji.

- i. Waombaji wenye sifa waambatishe nakala ya vyeti vya shule na vya taaluma, na cheti cha kuzaliwa. Hati za matokeo (result slip and testimonial/ provisional result havitapokelewa )
- ii. Waombaji wote waambatishe wasifu (CV) zao wakionesha namba za simu, anuani zao na wadhamini watatu.
- iii. Mwombaji aandike nyuma ya bahasha nafasi anayoomba
- iv. Waombaji wawe ni raia wa Tanzania na wawe na umri usiozidi miaka 45.
- v. Mwisho wa Kutuma maombi ni tarehe **08/04/2018 saa 10:00 jioni**
- vi. Waombaji watakaokidhi vigezo wataitwa kwa ajili ya usaili
- vii. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta, **hatutapokea maombi kwa njia ya mkono**
- viii. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri yaani [www.nsimbodc.go.tz](http://www.nsimbodc.go.tz)
- ix. Watakaofanikiwa kuitwa katika usaili (shortlisting) watafahamishwa kupitia matangazo, namba zao za simu na anuani za maombi yao.
- x. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALAMSHAURI YA WILAYA YA NSIMBO,  
S.L.P 688,  
MPANDA.**



Hamis Y. Mnubi  
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

**MKURUGENZI.MTENDAJI (W,  
NSIMBO**

Imetolewa na: